# NYOTA YA HUZUNI

Mwandishi: George Liwenga

Mchapishaji: Tanzania Publishing House

Mhakiki: M.S. Mponda.

Utangulizi: Hata kama mtunzi wa kazi ya Fasihi hatajitambua kuwa yuko katika daraja ya juu ya wananchi wa kawaida wa jamii yake, hadhira itamchukulia hivyo hadi hapo itakaporidhika kuwa matazamio hayo hayakufanikishwa na mtunzi mwenyewe. Kama kazi ya Fasihi iko katika maandishi, matazamio ya watu yatakuwa ni kuona matunda bora ya kazi ya sanaa. Matazamio hayo ni kiwango fulani cha burudani, uwezo wa mtunzi wa kutambua fikra na hisia za watu wa mazingira anayoyaandikia; kufahamu matatizo ya jamii hiyo na ikiwezekana njia sahihi ya kutatua matatizo hayo. Kwa kufanya hivyo basi atakuwa ameichambua na kuikosoa jamii na kuchochea hamasa ya kurekebisha makosa ambayo ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii yenyewe. Yote haya yanawezekana iwapo mwandishi ataitumia kwa tahadhari hazina ya sanaa aliyo nayo; ikiweka uzazi mzuri wa fani au sanaa na maudhui au mawazo makuu ambayo hadhira yake angependa iyazingatie. Na kwa vile fasihi ni sanaa ya lugha yenye lengo maalum, basi uwezo wa kuitumia lugha ni silaha kuu itakayompandisha au kumshusha daraja mtunzi.

Hali kadhalika, mhakiki naye ana dhima yake katika jamii inayotumia kazi ya Fasihi. Kama alivyo mwandishi, analazimika kuielewa jamii ambayo mwandishi anaiandikia na kuitumia jamii hiyo kama kigezo cha kupimia kufanikiwa au kuanguka kwa mwandishi. Aidha, ni dhima ya mhakiki pia kutoa ufafanuzi juu ya sehemu au vipengele ambavyo vikisomwa kwa jicho la juu juu pengine havitaeleweka vyema. Tahadhari moja juu ya lawama inayowapata wahakiki ni juu ya wahakiki kutoa 'maana isiyokusudiwa' na mwandishi. Lakini kwa kutumia misingi maalum ya kifasihi kama inavyoeleweka na jamii yenyewe, lawama hizi hubaki kuwa maji moto yanayokusudiwa yaunguze nyumba. Na kazi nyingine ya kutiwa maanani ifanywayo na mhakiki ni kutoa ushauri kwa waandishi na wachapishaji ya ubora wa kazi ya Fasihi ili ilete ufanisi zaidi machoni mwa mtumiaji wa kazi hiyo.

Kwa bahati mbaya sana, dhima hizi za wahakiki aghalabu huchukuliwa visivyo na baadhi ya watumiaji wa kazi za Fasihi. Watumiaji hao hujisahau kwamba mhakiki ameonesha tu mwanga unaoweza kuwaelekeza jinsi ya kuzama katika kazi ya Fasihi na kuibuka na maarifa ambayo yalihifadhiwa. Badala yake huuchukulia mwanga huo kuwa ndiyo maarifa yenyewe. Baya zaidi ni matumizi mabaya ya tahakiki kama yafanywavyo na ndugu zangu wanafunzi, hasa wale wanaokabiliwa na mitihani. Badala ya kufikiri kuwa tahakiki ni mchango tu unaomwezesha mtu kupanua fikra zake juu ya kazi ya Fasihi, baadhi yao(watahiniwa) hukusanya na kukariri tahakiki za vitabu mbalimbali na kuyanakili popote pale jina la kitabu hicho linapotokea katika swali la mtihani, bila kujali swali lenyewe linalenga kitu gani hasa! Kama hii ingekuwa dhima mojawapo ya tahakiki nisingekubali hata siku moja kuwapotezea watu wakati wao. Ikumbukwe kwamba tahakiki ni mwonjo na tafakari ya mtu au watu binafsi. Si jawabu ya hesabu ya mbili ongeza mbili. Ndiyo maana baadhi ya watu waliziita tahakiki zao Ndimi Zetu, Hisi Zetu, na kadhalika. Kukubaliana na mawazo ya mtu laweza kuwa jambo la kawaida, lakini lisichukuliwe kama ndio msingi wa maisha ya mtu. Kufanya hivyo ni kupunguza sehemu kubwa ya utu na kujikaribisha sana na ubandia. Nani angependa ajiite mtu-bandia!

Nyota ya Huzuni: Hii ni riwaya inayokusanya matukio mbalimbali yanayoibushwa hasa na mhusika mkuu, Bosi, katika mandhari ya Wilaya ya Mkurusi. Hii ni kazi ya sanaa, lakini yumkini kazi hii yaakisi matukio ya kihistoria ambayo yamewahi kutokea nchini Tanzania, hasa Tanzania Bara.

Mtunzi wa kazi hii anatumia wahusika wake katika kutupitisha katika mkondo wa matukio hayo na sababu zake. Hivyo ni muhimu kwa msomaji kuzingatia fikra na matendo ya wahusika hao ili kuielewa riwaya yenyewe.

WAHUSIKA

Bosi. Huyu ndiye mhusika mkuu na uti wa mgongo wa riwaya nzima. Yeye ndiye hasa nyota ya huzuni yaani nyota iliyoshusha huzuni miongoni mwa wananchi wa wilaya nzima ya Mkurusi. Bosi ni jina litokanalo na neno la Kiingereza "boss," neno ambalo maana yake ni 'bwana' mojawapo ya mtu atoaye amri pahala pa kazi. Hivyo kisaikolojia, bosi ameumbwa na sifa hiyo ya ubwana au utoaji amri katika jamii. Hali hiyo ya maumbile baadaye inajenga silika na azma ya maisha yake. Ananuia kuitekeleza azma hiyo hata kama gharama yake ni unafiki wa nafsi yake, fedheha, mateso na kupuuzwa kwa jamii yake. Tunapokutana na Bosi kwa mara ya kwanza twaambiwa ni Bwana Shauri katika Ofisi

ya Makokoto-Mkuu wa Wilaya. Hatajwi umri lakini yumkini ni kijana mdogo, aliyemaliza kidato cha nne, hajaoa bali ana kimada - Tatu. Ni mtu mwenye kiu ya ubwana mkubwa. Baadaye anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkurusi na anapata kimada mwingine - Dalia. Bosi ana ila nyingi zikiwa ni pamoja na ulevi, uzinzi, mwizi, ubadhirifu, ujambazi, kutokujali shida - hata za dharura, unafiki, udhalimu n.k. Baadaye anaachishwa kazi na Rais.

Makokoto - Huyu ni mwanamume wa makamo. Mkuu wa Wilaya. Mzinzi, mlevi, mbadhirifu, hajali kazi zake, mnafiki n.k. Kufunga safari isiyo ya lazima kunamnasa na kulazimika kuyatekeleza matakwa ya Bosi ya kuandikiwa 'ripoti nzuri' ya kazi. Makokoto anamsifu Bosi kijana hodari kwa vile anajua kula na wakubwa.(UK. wa 14) Hivyo twaweza kusema kuwa Makokoto ni rafiki mkuu wa Bosi.

Tatu: Ni msichana aliyekuwa kimada wa Bosi. Hatuambiwi juu ya wazazi wake wala jinsi walivyookotana na Bosi. Lakini Bosi anapojaribu kumtelekeza, anatumia mahakama kudai haki zake na anafanikiwa.(UK. wa 64-65) Ingawa ki-imani Tatu si mke wa Bosi lakini kwa mujibu wa sheria ana haki ya kutambuliwa na kutendewa kama mke.

Dalia: Huyu ni msichana anayesoma shule ya msingi. Ni mzuri wa sura na mshiriki katika kwaya ya shule yake. Anamvutia Bosi, na baadaye awa kimada wa Bosi baada ya wazee wa kijiji chake kumtoa kama kafara ili Bosi afurahi na awapatie maji. Kwanza anapinga uamuzi wa wazee wa kijiji wa kumtoa kafara. Baadaye anakubali kuwa kipenzi cha Bosi baada ya kurubuniwa kwa maneno na Bosi na wazee kuzidi kumtia chonjo kwamba kukubali kwake kwenda na Bosi kungewasaidia wazazi wake waliotiwa jela wafunguliwe.

Helena: Mwanamke mtu mzima. Anautumia mwili wake kama njia ya kumpatia kazi binti yake, Regina; mwuza pombe, kahaba wa Bosi.

Regina: Msichana mwenye ujuzi wa kupiga taipu. Ana sura ya kuvutia. Baadaye anagombewa na viongozi wilayani. Alikuwa bikira kabla ya kukutana na Bosi. Ni binti wa Helena.

Manyundo na Saidia: Matarishi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Wanyonge, lakini wanajitambua kuwa watu.

Kwetu: Mvulana mwenye elimu ya msingi. Ana mawazo ya ujasiri; alikuwa tayari kuanzisha na kuongoza mjadala juu ya kujinasua kutokana na madhara yaliyozushwa na Bosi kijijini kwao. Baadaye mratibu wa kuongoza ujumbe unaokwenda kumwona Rais huko Ikulu.

Madevu: Mzee wa kwanza wa kijijini kumwunga mkono Kwetu. Baadaye anateuliwa rasmi kuwa Mwenyekiti wa mazungumzo. Kisha anakuwa kiongozi wa msafara unaokwenda kumwona Rais.

Choso: Katibu Muhtasi wa Mkuu wa Wilaya ya Mkurusi baadaye anaachishwa kazi kwa kuonewa. Ni mwanamke mchapakazi. Lakini haonekani akichukua hatua za kujitetea.

Rais: Kiongozi wa nchi. Anadanganywa na Bosi juu ya siasa ya ujamaa na kujitegemea - anapofanya ziara ya wilaya ya Mkurusi. Ana tabia ya kutumia maagizo. Msikivu wa shida za wananchi na mpole. Hapendi viongozi wenye sifa za ubosi. Anamwachisha kazi Bosi baada ya kufahamu kuwa amedanganywa kwa muda mrefu.

Mandhari: Matukio ya hadithi hii hayakupewa mandhari yaliyochorwa wazi wazi. Badala yake msomaji anapata mwanga wa mbali juu ya mazingira ya hadithi. Mathalani, maisha ya mjini (Mkurusi) na ya vijijini hayaonekani kuwa ni tofauti hasa. Mengine ambayo si ya wazi ni hali ya hewa, umbile la nchi - kama milima, mabonde, mito n.k., haya yote ni muhimu katika kufanikisha maisha ya riwaya, kwani riwaya huyachukulia maisha kwa undani wake wote. Tunaoneshwa picha ya umasikini wa wanakijiji pale tuonapo vifurushi vyao duni baada ya vibanda vyao vya kupigwa mateke na kuteketezwa kwa moto.

Lugha: Mtunzi ametumia msamiati ambao umezoeleka katika mazungumzo ya watu wengi. Aghalabu mwandishi hatumii lugha ya mafumbo. Amejaribu kutumia misemo kama vile "Jambo likikupata patana nalo(uk. wa 33); alikuwa ameshiba jasho la wananchi(uk. wa 145); kula maharagwe ya bure(uk. wa 180). Mara chache kimejitokeza Kiswahili cha tafsiri, k.v. ndege walikuwa wakila matunda humo shambani. Aidha yapo matumizi ya misimu kama vile ...azimue mtungi wa jana - (uk. wa 10); masai mbili-(uk. wa 12) na tunataka tulibikiri sisi...(uk. wa 16).

Mtiririko wa matukio: Mtiririko wa matukio alioutumia mtunzi ni ule wa historia au wa moja kwa moja kama wengine tulivyozoea kuuita. Hadithi hii haikugawanywa katika sura mbalimbali, hivyo, inamuwia vigumu msomaji kuyazingatia anayoyasoma kikamilifu na bila uchovu. Kwa hadithi yenye kurasa zaidi ya 190, mtindo huu unachosha.

Hata hivyo matukio muhimu ni mipango ya safari ya Makokoto kuzuru wilaya yake; safari ambayo Bosi anajishirikisha bila kuipanga, alimradi nafasi imepatikana ya yeye Bosi kuambatana na mkubwa wake Makokoto. Tunapata kuifahamu tabia ya Bosi ya kufokea watu(uk. wa 3 - 4). Kabla ya safari na wawapo safarini tunashuhudia hali ya ulevi na uzinzi iliyowatawala viongozi hawa wawili.

Tunaambiwa kuwa kazi ya kuongea na wananchi inachukua dakika 10 tu. Wananchi wanachukia. Lengo la Bosi lapangwa uk. wa 14 na Makokoto analikubali,, 'Ripoti nzuri' inaandikwa

na taarifa ya habari inatangaza kupata Uongozi kamili wa wilaya ya Mkurusi.(Uk. wa 21).

Baada ya hapo Bosi analewa ulevi na analewa Cheo. Anakopa pesa za kununulia nguo zitakazofunika udhahiri wa unafiki wake. Anakopa pombe nyingi kwa sherehe ya kumshukuru Makokoto kwa wema wake. Bosi anapanga kanuni za utawala mpya wa kibosi. Baada ya hapo anapanga ziara ya kata zote 28 za wilaya yake.

Anapofika kijiji cha kwanza tu Bosi anampora Dalia na kuwatia mahabusu wazazi wa Dalia wanapodai kurejeshewa binti yao. Vyombo vya dola vyatumiwa ili kumlinda aendelee na uharibifu wake. Bosi anaungwa mkono na Afisaelimu - Mwalimu Mkuu anapojaribu kuwawakilisha wananchi, anafokewa na kupata adhabu ya kuhamishwa. Bosi amalizapo ziara yake tayari mwezi kamili umetimia. Hivyo anadai posho ya safari pamoja na mshahara wake. Arudipo ofisini hapana afanyacho. Katibu Muhtasi wake Choso anamsaidia baadhi ya kazi zake, jambo ambalo linamuudhi Bosi na kumwachisha kazi.

Ukurasa wa 90 - 100 kuna matukio mengi mchanganyiko, kama vile Bosi kukutana na Regina, binti wa rafiki yake - Helena; Bosi anashiriki katika wizi unaotokea katika duka la mwarabu (uk. wa 91); Bosi anamtumia Safi kama kisingizio cha uhujumu anajenga hoteli ya shilingi elfu 52(za wakati huo); Bosi anachukua fedha za wanakijiji kwa kuwadanganya angewapatia leseni ya biashara na bidhaa muhimu. Wakati huo huo Bosi anashirikiana na walanguzi.

Ukurasa wa 101 - 110 unatupa matukio mengine machafu: Bosi anawatia gerezani wachuuzi baada ya bibi yake kumweleza kuwa wachuuzi wanauza bidhaa kwa bei kubwa; Hakimu awaacha huru wachuuzi - Bosi achukizwa na kitendo hicho na kumpa uhamisho Hakimu; ubadhirifu, na kukiukwa kwa lengo la maisha ya Watanzania.

Ukurasa wa 113 na kuendelea twapata taarifa ya ziara anayokusudia kuifanya Rais wilayani Mkurusi. Bosi anaonekana akihangaika kutaka kumdanganya Rais. Tena, Bosi anavitumia vyombo vya dola na wananchi kwa jumla kupanga mipango ya kumdanganya Rais. Inadhihirika kuwa wilaya nzima ina vijiji vitano tu vinavyotambulika, na kamati ya dharura imekusudia kuunda vijiji 27. Hii ina maana kuwa kila kata ingekuwa na kijiji kimoja. Kwa upande wa ujamaa mjini, wananchi wamefunzwa kumdanganya Rais kwa kulifanya duka la bepari liwe la ushirika wa bandia.

Rais aitembelea wilaya ya Mkurusi na kupendezwa na yote yaliyotayarishwa kwa ajili ya ziara yake. Baada ya ziara,

viongozi wa wilaya wanafanya sherehe ya kufurahia "kazi yao nzuri". Lakini furaha hiyo yafuatiwa na maafa wakati Bosi anapogundua kwamba Rais hakufurahishwa sana na ukaaji wa wananchi katika vijiji. Ukurasa wa 153 - 180 tunashuhudia mipango ya kuwahamisha wananchi majira ya masika na kilimo. Uhamishaji ulifanyika kwa dharura na maandalizi yake ni sawa sawa na vita! Lakini anasa na ubadhirifu bado vinatawala mawazo na matendo ya viongozi.

Baada ya mateso haya wananchi wanaanza kutafuta umoja na kupeleka malalamiko yao kwa Rais na kumpasha ukweli jinsi alivyodanganywa na Bosi na viongozi wengine wa Mkurusi. Rais anamtuma Katibu wake na baada ya uchunguzi, inadhihirika kuwa Bosi alikuwa mwongo kwa kila alilosema na mnafiki kwa kila tendo. Aidha mateso ya wananchi yalisababishwa na yeye Bosi. Ndipo Bosi anapoachishwa.

Mfululizo wa matukio hayo unaonesha jinsi mtunzi wa riwaya hii alivyokuwa na mengi ya kutuambia. Wingi wa mawazo huenda ndio uliomfanya asahau hata baadhi ya kanuni za msingi katika uandishi wa riwaya.

Mawazo Makuu: Mwandishi wa riwaya hii alikuwa na mengi ya kutueleza. Baadhi ya mambo hayo ni:

1. Baadhi ya viongozi hupata madaraka kwa uhodari wao wa "kula na wakubwa wao" lakini maisha yao yote ni ya unafiki.

2. Watu wameshindwa kupata maendeleo kwa sababu ya viongozi wabaya ambao hawaelewi lengo la maisha yao binafsi na lengo la maisha ya jamii kwa jumla - mfano - Bosi na Makokoto.

3. Haifai kutegemea ripoti ya mtu mmoja kutoka mbali. Upendeleo na kuficha ukweli ni rahisi kufanyika.

4. Haki ya mtu wakati mwingine hupotea? Mfano: Wazazi wa Dalia wamefungwa, Dalia ameporwa, viongozi wengine wamehamishwa bila kupenda kwao lakini hadi Bosi anapoachishwa kazi hapana hata mmoja wao anayeonekana akiwa huru au kapata haki fulani aliyonyang'anywa.

5. Ulevi, kutowajibika, umalaya na ubinafsi ni maadui wakubwa wa maendeleo ya jamii.

6. Udhalimu unamtayarishia kaburi dhalimu mwenyewe. Bosi alikuwa dhalimu mkubwa. Lakini hatimaye udhalimu huo ndio unaomwangusha.

7. Wananchi wakiwa na umoja, watulivu, wajasiri na wakweli, wataweza kuuangusha ufashisti, udhalimu na kila uovu.

8. Si vyema kuvitumia vyombo vya dola isivyo halali kwa mfano matumizi mabaya yaliyofanywa na Bosi juu ya mahakama, magereza, jeshi la ulinzi n.k.

Haya ni baadhi tu ya yale ambayo yamejitokeza katika riwaya hii. Udhaifu na umaarufu wa riwaya hii waweza kuwa udhaifu na umaarufu wa mwandishi mwenyewe. Lakini hatuwezi kulaumu tu bila kusema mwandishi amefaulu kutuonesha baadhi ya mambo yanayokwamisha moto kwa kauli yake ya mashaka ya Rais: "...labda viongozi hao wanatakiwa waitwe na kueleweshwa mara kwa mara juu ya utendaji wa kazi zao na tabia nzuri kwa wananchi". Hapa mwandishi anajaribu kuonesha alivyo na sauti isiyo ya ukali dhidi ya kutokuweko kwa mipango mizuri na ufuatiliaji wa utendaji wa viongozi.